



## TANGAZO

### CRDB BANK PLC KUUZA HISA ZA KAWAIDA 435,306,432 KWA BEI YA SHILLINGI 350/= KWA KILA HISA

Kufuatia Azimio la kuuza Hisa Stahili lililopitishwa na Mkutano Mkuu wa Benki ya CRDB uliofanyika tarehe 9 Mei, 2015 na hatimaye kuidhinishwa na Mamlaka husika za usimamizi, Wakurugenzi wa Benki ya CRDB wanatangaza rasmi kuuzwa kwa Hisa Stahili kwa uwiano wa hisa moja (1) kwa kila hisa tano (5) za kawaida kwa Wanahisa watakaokuwemo kwenye daftari la Wanahisa hadi siku ya Alhamisi tarehe 18 Juni, 2015.

Uuzaji wa Hisa Stahili umedhaminiwa.

#### Ratiba ya Matukio Muhimu ni kama ifuatavyo:

Tukio	Tarehe
Tarehe ya Kufunga Daftari la Wanahisa	18 Juni, 2015
Kusambaza Waraka wa Maelezo na Barua ya Mgao wa Awali kwa Wanahisa wenye sifa	22 Juni, 2015
Kuanza kwa zoezi la kuuza Hisa Stahili	26 Juni, 2015
Tarehe ya Mwisho ya Kuuza Hisa Stahili	16 Julai, 2015
Kutangaza Matokeo	10 Agosti, 2015
Kuorodhesha na Kuanza biashara katika soko la hisa la Dar es Salaam (DSE)	14 Agosti, 2015

Kwa taarifa zaidi, Wanahisa wanashauriwa kusoma kwa kina Waraka wa Maelezo na Barua ya Mgao wa Awali zitakazotumwa kwao. Waraka wa Maelezo unaweza kupatikana katika Matawi yote ya Benki ya CRDB yaliyoko nchini, Soko la hisa la Dar es salaam (DSE) na kwenye Ofisi za Mawakala wa mitaji na dhamana. Pia Muhtasari wa Waraka wa Maelezo unapatikana kwenye tovuti ya Benki kwa anuani hii: [www.crdbbank.com](http://www.crdbbank.com)

**Kwa Agizo la Bodi**

**Katibu wa Kampuni**  
16 Juni, 2015